

Swahili transcript:

Nicholas: Labda kwamba unafikiri kwamba ni dhana sawa ambayo inatakiwa iendelee kusukumwa kwa watu waendeleo kuhimizwa au wafuatilie ama itafutwe njia nyingine labda, kitu kingine ambacho kitawawezesha kuweza kushiriki katika ukuaji wa uchumi?

Andrew: Mimi naona kwa sasa hivi itabidi tu, sidhani kama kuna choice, itabidi tu kwa namna moja au nyingine itabidi tujizoeze tu kwamba inabidi tuanze kujijiri wenyewe, kuanzisha biashara, kuanzisha makampuni, kutokana na fields zetu, utaalamu ulioupata chuoni uutumie ili kuanzisha kampuni au kitu chochote ambacho by then kitakuja ku-generate ajira kwa watu wengine, wataalam wenzako au hata watu ambao ni unskilled labour, eeh!. Kwa sababu ukiangalia kama soko la ajira linajaa sasa hivi serikali haiwezi tena kuwa inategemea kuwa inaingiza watu wote wanaomaliza, kwa sababu ni zaidi ya ambao serikali inawahitaji. Kwa hiyo moja kwa moja itabidi sisi wenyewe watu ambao tumepata nafasi ya kusoma chuo, tuanze kuanzisha ajira kwa ajili ya wenzetu, vijana wenzetu ambao hawakupata elimu kama tuliyopata sisi. Hata kama itakuwa vigumu mwanzoni, nadhani hata tukisema kufungua hii mipaka ya Kenya na Uganda, itasaidia ile kutuonyesha, kufungua mwanga kwa sababu wao hawakuwa kwenye system kama ya kwetu ya ujamaa ambayo ilikuwa serikali inafanya kila kitu. Kitu chochote ambacho ni cha kitaalam, kitu chochote ambacho kilihitaji exposure na na mambo ya international sijui nini ilikuwa inafanywa na serikali. Sasa hivi, mtu kama unataka kuwa na kampuni, inabidi mwenyewe uwe na uwezo wa kupata information zote ambazo serikali ilikuwa ina uwezo wa ku-acquire, kwa sababu serikali inakuwa na link ya wataalam wengi.

English translation:

Nicholas: Do you think it is okay to continue to inform citizens about how they can help in one way or another to improve our economy? Or should we look for other ways to enable people to participate in its growth?

Andrew: There is no choice; we should participate in improving our economy by creating jobs and establishing our own companies and businesses according to our fields. The knowledge you got in college should enable you to start a company that will generate employment for other people...skilled people like you or even unskilled labor. Many people are graduating from colleges, and the government will not be able to employ them all because the number exceeds what the government needs. We who had the opportunity to get education up to the university level are responsible for creating jobs for our fellow youth who didn't have a chance for higher education. It will be difficult at the start. When we establish the East African employment market, it will open our minds. This is because Kenya and Uganda were not under the socialism policy we had. Our policy made the government do everything for its citizens. Everything professional or that which needed

international exposure was carried out by the government. Now if you want to establish a company, you can get all the information you need to start your own business. Before, it was done by the government.

About CultureTalk: CultureTalk is produced by the Five College Center for the Study of World Languages and housed on the LangMedia Website. The project provides students of language and culture with samples of people talking about their lives in the languages they use everyday. The participants in CultureTalk interviews and discussions are of many different ages and walks of life. They are free to express themselves as they wish. The ideas and opinions presented here are those of the participants. Inclusion in CultureTalk does not represent endorsement of these ideas or opinions by the Five College Center for the Study of World Languages, Five Colleges, Incorporated, or any of its member institutions: Amherst College, Hampshire College, Mount Holyoke College, Smith College and the University of Massachusetts at Amherst.

© 2003-2008 Five College Center for the Study of World Languages and Five Colleges, Incorporated